



**“KUKUZA IMANI NA MATUMAINI KATIKA NYAKATI ZETU”**

## MASWALI KABLA YA MKUTANO 2019

- Majibu yetu yawe ya kweli na yaeleze uhalisia wa mambo;
- Yafike kwa njia ya barua pepe kwa Rais ama Katibu Mkuu;
- Yajibiwe na kutumwa na kila Kikundi cha Wanaverniana; Rais wa Kanda ataambatanisha maelezo yake mafupi;
- Maswali yanahu mada ya MATUMAINI KWA AJILI YA MUSTAKABALI katika nyanja/vipengele vifuatavyo: a) karama, b) Chama, c) Familia Verniana kwa ujumla d) mazingira tunapoishi;
- Majibu yote yatafanyiwa kazi na Kamati ambayo bado haijaundwa; katika Kamati hiyo, lakini, atakuwepo Rais;
- Majibu hayo yatasaidia kuandaa “mwongozo wa kazi”, utakaosahishwa na Kamati Kuu kabla ya mkutano na ambao utasomwa na kufanyiwa kazi kwenye mkutano na utasaidia kuandaa Mpango wa Chama wa miaka 4 ijayo;
- Maswali haya yatatumwa kabla ya mwisho wa mwezi Novemba kwa Wenyeviti wa Kanda na Wanakamati wao, kwa Mwenyekiti wa kila Kundi na kwa Walei ambao tuna anwani zao; majibu yote yanapaswa kurudishwa kabla ya tarehe 15 machi 2019;
- Maswali yatatumwa pamoja na Maelezo yake.

### Kipengele juu ya karama

1) *Unaishi kila siku karama ya kiverniani?*

**SANA KIDOGO HATA KIDOGO**

a) *Elezza sababu za jibu lako*

b) *Endapo umejibu SANA au KIDOGO eleza unaiishi NAMNA GANI (kupitia sala, kazi, ushuhuda...)*

2) *Unahitaji kuelewa zaidi karama ama umeshai lewa ya kutosha?* **KUELEWA ZAIDI      TAYARI NAIISHI**



a) Se Nedapo unahitaji kuelewa zaidi na kupanya zaidi ndani ya karama, ni kwa namna gani unadhani unaweza kufaulu katika hilo?

b) Unashuhudia karama na unaweza kuieleza hata kwa wengine?

NDIYO	NAJITAHIDI	NASHINDWA
-------	------------	-----------

c) Namna gani?

3) Ndani yako, unayo matumaini kuwa karama ya kiverniani inaweza kupanya na kustawi katika nyakati zetu na katika sehemu mbali mbali tunapoishi? SANA KIDOGO HATA KIDOGO

a) Kwa nini? Kwa namna gani?

#### Kipengele juu ya Chama

4) Chama cha kiverniani kimetimiza miaka 15 tangu kuanzishwa na sasa kinajiardaa kuadhimisha mkuutano mkuu wa V: je, kimetimiza matarajio yako? NDIYO KIDOGO HATA KIDOGO

5) Upande wa malezi, unaonaje malezi tunayotoa?

MAZURI	YANATOSHA	HAYATOSHI
--------	-----------	-----------

a) Endapo unaona kuwa malezi yanahitaji kuboreshwa zaidi, yapi ni mapendekezo yako?

b) Yapi yalikuwa matarajio yako kimalezi?



**6) Una matarajio yapi kwa nyakati zijazo?**

**7) Je, Chama kinaweza kukua na kuwa imara zaidi? NDIYO KIDOGO HAPANA**

a) Fafanua....

b) Ukiwa umejibu KIDOGO au HAPANA, una mapendekezo yapi ili Chama kikue zaidi? Kwa njia gani na nyenzo zipi?

#### **Kipengele juu ya Familia ya kiverniani**

Mara nyingi tumesigitiza kukuza roho ya kifamilia, pamoja na Masista na Wamisionari wa Upendo. Tumepiga pia hatua nyingi, huko Argentina, Lebanon na Italia.

**8) Je, tunaendelea vizuri katika jitihada hizo? NDIYO LABDA BADO**

a) Fafanua...

b) Pamoja na kushirikishana katika malezi, sala na utume, tunahitaji kupiga hatua gani?

c) Una matumaini na matarajio yapi katika hilo?

#### **Kipengele juu ya mazingira/nyakati tunapoishi**

Dunia ya leo inaonekana kama dunia inayoishi bila Kristo, bila hata tunu za kawaida; miito na wafanyakazi katika shamba la Bwana wamepungua. Katika mazingira haya,

9) endapo Mapadre hawapo karibu na makanisa hayapo karibu unaweza kuishi matumaini ya kikristo?

SANA KIDOGO HATA KIDOGO



## *Chama cha Walei Wanaverniani*



a) Unaweza kufanya nini, kama Mlei Wanaverniana, katika changamoto hiyo?

b) Katika safari ya matumaini, kwako ni muhimu undugu/jumuiya/kundi?

SANA KIDOGO HATA KIDOGO

c) Fafanua...

10) Ukiwa unashindwa kushuhudia na kutangaza imani na matumaini ndani ya Familia yako (ya kiverniana), basi maisha yako ya kiroho yatakuwa ya namna gani?

**KAMATI KUU YA WALEI WANAVERNIANA**